Ethical Trading Initiative



# Kanuni za Mpango wa Jinsia Katika Kilimo (GAIA) za Kukomesha Dhuluma ya Kijinsia na Unyanyasaji Katika Kilimo cha Biashara na Uvuvi

**Muhtasari**



## Maana ya GBVH

Dhuluma ya Kijinsia na Unyanyasaji (GBVH) ni ukatili au unyanyasaji kulingana na jinsia ya mtu - iwe mwanaume au mwanamke. Hii ni pamoja na ukatili au vitisho vya ukatili. Unyanyasaji ni mwenendo wa kimwili, wa maneno au usio wa maneno unaoelekezwa kwa mtu, ambao unamfanya ahisi wasiwasi, kutishwa, kukerwa au kudharauliwa kazini.

GBVH ni tabia mbalimbali kama vile kupiga kelele, kuwatukana wafanyakazi, kushika mtu bila ridhaa au kuwakejeli kwa kutumia lugha ya kingono. Mifano ya tabia mbaya zaidi ni dhuluma ya kijinsia na kuomba upendeleo wa kingono kwa kubadilishana na kupewa kazi, kufanya upya mikataba au majukumu mepesi, iwe wakati wa kuandikishwa au kuajiriwa na unyanyasaji wa kingono.

## GBVH inatuathiri sote

GBVH imeenea sana na inaweza kumpata mtu yeyote, ikiwemo wanaume, lakini inaathiri wanawake kwa kiasi kikubwa zaidi.

Biashara zina jukumu la kuhakikisha usalama wa wafanyakazi wao wote pamoja na wageni wanaotembelea sehemu zao za kazi, ikiwemo wanaotafuta kazi, wafanyakazi wa muda au waliopewa kandarasi za muda. Biashara zina jukumu la kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayesababisha GBVH wakati anazifanyia kazi, ikiwemo wahusika wengine kama vile watoa huduma za kazi, walinzi au mawakala wa uajiri.

> ***Kanuni za GAIA ni mfumo wa kuoanisha na kuratibu hatua za kuzuia na kukabiliana na GBVH mahali pa kazi.***

GBVH haiathiri wafanyakazi pekee; huathiri pia biashara. GBVH inaathiri utendaji kazi wa wafanyakazi kwa kusababisha ukosefu wa usalama, ugomvi na kiwango cha juu cha wafanyakazi kuacha kazi. Kinyume chake, wafanyakazi wanaojihisi wako salama na kuheshimiwa kazini hufanya kazi kwa bidii na utulivu zaidi. Biashara pia zinaweza kupata uharibifu wa sifa, athari za kisheria kutokana na matukio na gharama za kifedha zinazohusiana na kujibu kesi na kurekebisha makosa/shida.

## Kanuni zilizoundwa kwa pamoja

Kanuni za GAIA ni mfumo wa kupanga pamoja na kuweka utaratibu hatua za kuzuia na kukabiliana na GBVH mahali pa kazi. Zimeandaliwa kwa kushirikiana na wawakilishi mbalimbali kutoka kwenye biashara na mashirika ya watu binafsi (ikiwemo vyama vya wafanyakazi na mashirika yasiyo ya kiserikali), serikali na taasisi na mipango ya kimataifa kulingana na uzoefu wao wa kushughulikia GBVH.

# Kanuni za GAIA

1. Aina zote za dhuluma za kijinsia na unyanyasaji zimepigwa marufuku

2. Biashara zinajizatiti kuzuia GBVH na kuhakikisha washirika wao wa biashara wanafanya vivyo hivyo

3. Uongozi andamizi unazingatia athari za hatari za GBVH za maamuzi yote ili kuhakikisha maeneo ya kazi yana usawa, yenye heshima na yasiyo na GBVH

4. Sera na taratibu zimeundwa na kutekelezwa ili kuzuia GBVH mahali pa kazi

5. Mazoea ya ununuzi wa kuwajibika huwezesha uchukuliwaji wa hatua dhidi ya visababishi vya msingi vya GBVH na kusaidia uzalishaji endelevu

6. Wafanyakazi wameajiriwa katika kazi nzuri kupitia kufanya maamuzi kwa uwazi

7. Biashara huwawezesha wafanyakazi kutumia haki na majukumu yao katika mahali pa kazi pasipo na GBVH

8. Wafanyakazi wote wanaamini kwamba wanaweza kuripoti GBVH kwa siri au bila kujitambulisha, bila hofu ya kulipiziwa kisasi

9. Biashara kutoa suluhisho la GBVH na kuwawajibisha wakosaji

10. Biashara zinawajibika kwa GBVH na kujifunza kutokana na hatari na ripoti za GBVH



## Zinatumika kwa biashara zote katika shughuli zao wenyewe na mnyororo wa ugavi

Biashara zinapaswa kufuata kanuni hizi wakati wa kuandikisha na kuajiri wafanyakazi na wakati wa kununua bidhaa na huduma kutoka kwa biashara zingine ili kuhakikisha kila mtu anaelewa na anajua kinachohitajika ili kukabiliana na GBVH.

## Kile kitakachohitajika ili kuleta mabadiliko

Kanuni hizi zinaelezea matokeo ambayo biashara zinapaswa kujitahidi kuyafikia katika shughuli zao na mnyororo wa ugavi. Zimejikita katika **uhuru wa ushirikiano,** zinaambatana na viwango vya kimataifa na zinasisitiza hatua za pamoja.

## Ili kuwa na uhakika kuwa unafanya mabadiliko ya kweli, shirikiana na wataalamu

Biashara zinapaswa kushughulikia GBVH pamoja na wafanyakazi na wawakilishi wao/vyama vya wafanyakazi. Wafanyakazi wanaelewa vizuri zaidi hatari zinazowakabili. Kwa sababu kazi zao zinategemea mafanikio ya biashara, wao ni washirika wenye motisha na wenye kujenga.

**Wafanyakazi waliojipanga wenye uwakilishi thabiti na uongozi kutoka kwa wanawake, wanaweza kushirikiana na biashara ili kutambua hatua mahususi za kuzuia GBVH na wanaweza kuunda maeneo salama ya kazi kupitia sera, taratibu na mikataba ya majadiliano ya pamoja (CBAs).**

GBVH inaweza kuwa tata sana na ngumu kushughulikia – wataalamu wa GBVH, vyama vya wafanyakazi, mashirika ya haki za wanawake na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yana maarifa na ujuzi wa kuwasaidia waathiriwa na wanusurika ambayo biashara zinaweza kukosa.



## Hatua zinapaswa kuwa:

- Zimepewa kipaumbele kulingana na **hatari kubwa zaidi au athari za GBVH kote katika shughuli za biashara na minyororo ya ugavi.**
- Kulingana na **ushiriki wa washikadau muhimu** na wale ambao wameathiriwa na walio katika hatari ya GBVH, wafanyakazi, hasa wanawake na wawakilishi wao, na watu binafsi na mashirika yenye utaalamu wa GBVH. Hii ni pamoja na kuzingatia mahitaji na matakwa ya **waathiriwa na manusura katika mchakato wote.**
- Kuelekezwa kwenye **kuzuia, kulenga wakosaji na visababishi vya msingi vya GBVH.** Hii ni pamoja na kushughulikia kanuni za msingi, imani na mitazamo, tofauti za kimamlaka zinazotokana na miundo ya mahali pa kazi na udhaifu unaosababishwa na malipo duni na kazi chache, isiyo salama, inayoendeshwa na mnyororo wa ugavi na mienendo ya soko.

## Kanuni za upatanifu, majadiliano na vitendo

Sote tunataka mazingira salama na yenye heshima ya kazi kwa ajili yetu na wengine. Kanuni zinapaswa kuchochea majadiliano na tafakari kati ya biashara na washirika wao (wagawaji, wanunuzi, wakandarasi wadogo, wahusika wengine na kadhalika) kuhusu jinsi ya kuzuia GBVH mahali pa kazi.

Hii inahitaji juhudi za pamoja, ikiwemo kugawana gharama na rasilimali kwa haki. Biashara zinaweza kutumia kanuni hizi kuratibu vitendo vyao, kuunganisha rasilimali na kuepuka marudio .

Kwa mfano, wazalishaji na wakulima wanaweza kutumia hizi kutambua na kuomba usaidizi wanaohitaji kutoka kwa wauzaji rejareja na wagawaji ili kuzuia GBVH na kuratibu juhudi na watoa huduma za kazi za pamoja ili kuboresha mifumo ya malalamiko. Wauzaji rejareja na wagawaji wanaweza kutambua fursa za kuongeza mafunzo na usaidizi kwa washirika wao katika eneo au sekta.

> *Hii inahitaji juhudi za pamoja, ikiwemo kugawana gharama na rasilimali kwa haki.*

Wauzaji rejareja wanaweza kutathmini hatari kwa wafanyakazi waliopewa kandarasi katika maghala yao na kupatanisha ujumbe kwa washirika wao wa kawaida wa biashara na kuunganisha rasilimali ili kusaidia juhudi za kuzuia na kurekebisha.

## Unda nafasi ya uwazi

- Biashara zinapaswa kuwasaidia washirika katika safari yao ya kuboresha mazoea yao. Ufichuzi wa uaminifu wa changamoto unaofanywa na biashara zilizojitolea kukabiliana na GBVH na visababishi vyake vya msingi unapaswa kuungwa mkono na washirika wao.
- Wafanyakazi, vyama vya wafanyakazi na mashirika mengine ya kiraia yanaweza kutumia kanuni hizi kama msingi wa kushirikisha biashara kuhusu suluhisho.
- Biashara zinaweza kuonyesha kujitolea kwao kuzuia GBVH na kuunda maeneo salama ya kazi kupitia uwazi kwa wafanyakazi, washirika wao na umma. Kujadili kuunda nafasi na kuashiria utayari wa mazungumzo huwezesha uwajibikaji na ushirikiano zaidi na maendeleo.

**Rasilimali kwenye GAIA**

- Kanuni za GAIA
- Maswali yanayoulizwa mara kwa mara (FAQs)

Pata maelezo zaidi

# Muhtasari

## 1 Aina zote za dhuluma za kijinsia na unyanyasaji zimepigwa marufuku

Hizi ni tabia mbalimbali zinazoelekezwa kwa mtu kulingana na jinsia yake, ikiwemo vurugu au vitisho vya vurugu na mwenendo wowote wa kimwili, wa maneno au usio wa maneno, ambao unamfanya ahisi wasiwasi, kutishwa, kukerwa au kudharauliwa katika mazingira yake ya kazi au shughuli zinazohusiana na kazi.

Mtu yeyote anayefanya kazi au anayehusishwa kwa biashara anapaswa kufahamu wazi kwamba GBVH iliyofanywa kwake au naye haitavumiliwa. Kila mtu analindwa ikiwemo wanaotafuta kazi, wafanyakazi wa msimu/wa kawaida na wa kudumu, wafanyakazi wahamiaji na wafanyakazi wa mkataba.

- Washirikishe mapema wafanyakazi katika mazungumzo kuhusu GBVH ili kuhakikisha kuelewa kwao kunaambatana na sera ya biashara na kinyume chake. Jenga utamaduni wa kuzuia na kuheshimu kulingana na maadili ya pamoja ya heshima, haki na usawa. Himiza mazungumzo ya wazi na nafasi salama za kuripoti kupitia shughuli za mara kwa mara za uhamasishaji na mafunzo.

## 2 Biashara zinajizatiti kuzuia GBVH na kuhakikisha washirika wao wa biashara wanafanya vivyo hivyo

Wanafanya uchunguzi wa kina wa haki za binadamu unaozingatia jinsia, kukuza ushirikiano na kushiriki wajibu, hatari na gharama kwa haki.

Kwa sababu ya uhusiano wao wa kibiashara, biashara zina jukumu la kushirikiana na washirika wao kushughulikia GBVH kwa kutoa usaidizi, mafunzo na kushiriki rasilimali, ikiwemo ufadhili unaohitajika.

- Jumuisha sera zinazohusiana na GBVH na matarajio ya pande mbili katika mikataba, ikihitaji washirika kuweka viwango sawa kwa washirika wao. Shirikiana na biashara nyinginezo ili kupatanisha juhudi na wafanyakazi, vyama vya wafanyakazi na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs).

## 3 Uongozi andamizi unazingatia athari za hatari za GBVH za maamuzi yote ili kuhakikisha maeneo ya kazi yana usawa, yenye heshima na yasiyo na GBVH

Wanazingatia athari za shughuli za biashara katika shughuli zao wenyewe na mnyororo wa ugavi.

Bila kujali ukubwa wa biashara au eneo katika mnyororo wa ugavi (kwa mfano wazalishaji, wagawaji, wanunuzi, wakandarasi na kadhalika), wamiliki na usimamizi andamizi wana jukumu la kushughulikia GBVH.

- Unganisha udhibiti wa GBVH kama hatari kwa haki za binadamu za wafanyakazi na kwa biashara katika kufanya maamuzi, na rasilimali (binadamu na kifedha) ili kufanya hivyo.

## 4 Sera na taratibu zimeundwa na kutekelezwa ili kuzuia GBVH mahali pa kazi

Sera na taratibu zinahitaji kuwa wazi kuhusu kile kinachochukuliwa kuwa tabia inayokubalika na isiyokubalika mahali pa kazi, jinsi GBVH itakavyozuiwa, jinsi inavyoweza kuripotiwa na jinsi itakavyoshughulikiwa kwa njia nyeti, salama na ya haki kwa mwathiriwa, manusura na mtuhumiwa wa uhalifu.

- Jumuisha wafanyakazi na wawakilishi/vyama vya wafanyakazi katika kutunga na kuendeleza sera na taratibu na ushirikiane nao kuhusu jinsi utekelezaji unavyoendelea. Wafundishe mara kwa mara wafanyakazi wote, ikiwemo usimamizi kuhusu sera na taratibu hizi.

## 5 Mazoea ya ununuzi wa kuwajibika huwezesha uchukuliwaji wa hatua dhidi ya visababishi vya msingi vya GBVH na kusaidia uzalishaji endelevu

Mazoea ya ununuzi wa kuwajibika – ikiwemo utabiri, mikataba, kuagiza, muda, bei na masharti ya malipo, yanapaswa kuwasaidia washirika kusimamia shughuli kwa uendelevu, kuwezesha kazi nzuri na uwekezaji katika kuzuia.

- Tathmini ikiwa mazoea ya biashara, ikiwemo bei, yanasaidia washirika kutoa mazingira mazuri ya kufanyia kazi, mishahara ya kujikimu na usalama wa kazi, na kukidhi viwango vya kijamii na mazingira. Tambua na usaidie washirika ambao wana uwazi na wamejitolea kushughulikia GBVH.

## 6 Wafanyakazi wameajiriwa katika kazi nzuri kupitia kufanya maamuzi kwa uwazi

Hatari ya GBVH huongezeka wakati uthabiti wa kazi na malipo hayatoshi kutimiza mahitaji ya wafanyakazi.

- Toa kazi zenye malipo ya haki kulingana na ushirikiano na wafanyakazi na wawakilishi wao/vyama vya wafanyakazi. Andikisha moja kwa moja na utoe kazi salama kadiri inavyowezekana. Hakikisha uwajibikaji na uangalizi wa maamuzi yanayohusiana na malipo ya wafanyakazi na hali za kazi, na hivyo kupunguza fursa kwa watu binafsi kutumia vibaya uwezo na mamlaka yao. Shirikiana na wahusika wengine kama vile watoa huduma za kazi na wakandarasi ili kuhakikisha wanazingatia majukumu ya kuzuia GBVH.

## 7 Biashara huwawezesha wafanyakazi kutumia haki na majukumu yao katika mahali pa kazi pasipo na GBVH

Kuzuia GBVH kunahitaji utamaduni thabiti wa haki, usawa na kutovumilia kabisa mahali pa kazi. Wafanyakazi wanapaswa kuelewa haki zao na sera mahususi za mahali pa kazi na wahisi kuwa na uwezo wa kuripoti tabia isiyofaa iwe inaelekezwa kwao au kwa wengine kama watazamaji hai.

- Hakikisha wafanyakazi wote wanaarifiwa na kufundishwa kuhusu haki zao za kazi na usimamizi una vifaa vya mazungumzo bora ya kijamii na majadiliano ya pamoja. Endeleza usawa wa kijinsia kupitia mazoea jumuishi na kuunda sehemu salama kwa wafanyakazi wote, hasa wanaume na wale walio kwenye mamlaka, kukanusha imani, mitazamo na kanuni zinazochangia GBVH.

## 8 Wafanyakazi wote wanaamini kwamba wanaweza kuripoti GBVH kwa siri au bila kujitambulisha, bila hofu ya kulipiziwa kisasi

Wafanyakazi wanapaswa kujua kwamba ripoti zinashughulikiwa kwa heshima, unyeti na haki ili kujenga imani yao katika mifumo ya malalamiko.

- Hakikisha kuna njia nyingi za kuripoti kwa mshughulikia kesi aliyehitimu ambaye hayupo chini ya ushawishi wa wanaodaiwa kuwa wakosaji na vipaumbele vya biashara. Chukulia ripoti zote kwa uzito na kuelezea kwa uwazi kila hatua kwa aliyeripoti na upate kibali kutoka kwake kabla ya kuendelea ili kuzuia madhara yasiyotarajiwa.

## 9 Biashara kutoa suluhisho la GBVH na kuwawajibisha wakosaji

**Wanatumia mbinu inayolenga mwathiriwa na manusura na kutumia taratibu za nidhamu za haki kwa wakosaji.**

Urekebishaji unapaswa kulenga kumrejesha mwathiriwa au manusura katika nafasi ambayo angekuwa iwapo GBVH haingetokea.

- Hatua zinapaswa kuongozwa na mahitaji, usalama na matakwa ya waathiriwa na manusura, kuwawajibisha wakosaj bila kujali nafasi yao na kuchukua jukumu la mapungufu yoyote au maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa katika biashara.

## 10 Biashara zinawajibika kwa GBVH na kujifunza kutokana na hatari na ripoti za GBVH

Biashara zinawajibika kuripoti jinsi ambavyo zimetimiza jukumu lao la kushughulikia GBVH.

- Fuatilia na utathmini mara kwa mara juhudi za kuzuia na mwitikio na wafanyakazi na wawakilishi wao/vyama vya wafanyakazi. Ripoti kwa uwazi kuhusu maendeleo, shiriki changamoto na mafunzo na washirika na utambue fursa za ushirikiano ili kupata suluhisho kwa visababishi vya msingi vya GBVH.


Ethical Trading Initiative

ETI is a leading alliance of NGOs, trade unions, and companies advancing human rights in supply chains.

Our vision is of a world of work that protects human rights, ensures dignity for all, provides opportunity and is free of exploitation and abuse.



**Ethical Trading Initiative**
LHBO4 Kennington Business Park
1-3 Brixton Rd, London SW9 6DE
United Kingdom

+44 (0)20 7841 4350

ethicaltrade.org

info@eti.org.uk

LinkedIn